



TAARIFA KWA UMMA
HAFLA YA KUSAINI MKATABA WA UJENZI WA MRADI WA ULAZAJI BOMBA LA MAJI
KUTOKA KIBAMBA HADI KISARAWE

Katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli la kuupatija mji wa Kisarawe maji kutoka katika Mtambo wa Ruvu Juu, leo hii Mkandarasi China Henan International Cooperation Group ametia saini mkataba wa ujenzi na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASA). Gharama ya mradi mzima ni shilingi 10,849,788,087.50.

Utiaji saini wa Mradi huu unashuhudiwa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Inj. Isack Kamwelwe (Mb) na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Selemani Jafo (Mb).

Mradi utatekelezwa kwa muda wa miezi 15 kuanzia tarehe ya kusaini mkataba na mkandarasi atakuwa na muda wa miezi 12 ya uangalizi na marekebisho baada ya mradi huo kukamilika. Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa sehemu kubwa ya vifaa vya mradi hususan mabomba yatanunuliwa katika viwanda vilivyopo ndani ya nchi na hivyo kuchangia katika kuimarisha uchumi wa nchi. Mkandarasi atakuwa na ajira za muda mfupi wakati wa ulazaji wa Bomba na ujenzi wa Matenki. Hii ni fursa kwa Wananchi wa Kisarawe na Pwani kwa ujumla.

Lengo la mradi huu ni kupeleka maji lita 4,080,000 kwa siku na kazi zitakazohusika ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji kitakachokuwa na uwezo wa kufungwa pampu nne, ununuzi na ufungaji wa pampu mbili zenye uwezo wa kusukuma maji kiasi cha lita 60 kwa sekunde kwa kima cha mita 180 na kujengwa kwa kituo cha kupokea maji chenye uwezo wa kuhifadhi lita 480,000. Mji wa Kisarawe upo katika muinuko na ili maji yaweze kufika kutoka katika tenki la Kibamba kituo cha kusukuma maji kitahitajika kujengwa.

Mradi pia utahusisha ununuzi na ulazaji wa mabomba makuu ya chuma kipenyo cha milimita 400 kwa umbali wa kilometa 17 kwenda katika Makao Makuu ya Wilaya na bomba lenye kipenyo cha milimita 300 kwa umbali wa kilometa 5.3 kutoka katika bomba kuu kwenda Vigungu na bomba lenye kipenyo cha milimita 200 kwa umbali wa kilometa 9 kutoka Vigungu kuelekea eneo lililotengwa kwa ajili ya viwanda. Aidha mtandao wa mabomba ya plastiki ya ugawaji maji ya kipenyo kati ya milimita 90 hadi 200 kwa urefu wa kilometa 29 yatalazwa katika maeneo mbalimbali ili kuboresha usambazaji maji kwa watumiaji wa maji Mjini Kisarawe.

Hata hivyo, pamoja na mradi huu mkubwa, katika hatua ya muda mfupi ya kupunguza tatizo la maji katika mji huo, Wizara ya Maji kupitia DAWASA inatekeleza mradi wa maji wa Vigama ambapo kisima kipya kimechimbwa. Mkandarasi wa kufunga pampu, kujenga mnara, kufunga tenki la kuhifadhi maji na kulaza mabomba la kusambaza maji hayo alianza kazi mwezi Februari 2018. Mradi huu unatarajia kukamilika tarehe **30 Juni 2018**. Mvua kubwa za Masika zinazoendelea nchini kote umepunguza kasi ya mkandarasi.

Aidha DAWASA inatarajia kukarabati kisima cha Shule ya Sekondari Maneromango ikiwa ni mchango wake katika mkakati wa kuboresha miundombinu ya shule ili kuongeza ufaulu katika Wilaya hiyo. Utaratibu wa kumpata mkandarasi wa kazi hii upo katika hatua za mwisho na matarajio ni kuanza kazi hii mwezi huu (Mei) 2018.

Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano wa Jamii
DAWASA